



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

CHUO CHA MAJI



TANGAZO KWA WAHITIMU WA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Ofisi ya Afisa Huduma kwa Wanafunzi (Student Support Officer), Chuo cha Maji, inawatangazia wahitimu wote wa mwaka wa masomo 2025/2026 kuwa wanatakiwa kupakua orodha ya majina ya wahitimu kupitia tovuti rasmi ya Chuo cha Maji na kuhakiki usahihi wa majina yao kwa kuyalinganisha na majina yaliyo kwenye vyeti vyao vya kidato cha Nne.

Wahitimu ambao watabaini kuwa majina yao katika orodha hiyo yanatofautiana na majina yaliyo kwenye vyeti vyao vya kidato cha Nne, wanatakiwa kutoa taarifa haraka iwezekanavyo kupitia barua pepe dass@waterinstitute.ac.tz kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho stahiki.

Vile vile, wahitimu ambao majina yao hayapo kwenye orodha hiyo, wanatakiwa kutoa taarifa kupitia barua pepe tajwa hapo juu.

Taarifa zote zinapaswa kuwasilishwa kabla ya tarehe 2 Novemba 2026.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko

28 Oktoba 2026